



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Kumi na Saba – Tarehe 20 Mei, 2022

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2022/2023.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka 2022/2023.

II. MASWALI:

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

155. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Ni kwa kiasi gani Serikali imeweza kupunguza utegemezi wa kuagiza bidhaa mbali mbali kutoka nchi za nje kwa kutumia bidhaa zinazozalishwa na vyuo vya amali nchini kwetu.

Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

96. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa kuwa changamoto ya upatikanaji wa maji safi na salama inaonekana kuwa bado ni kubwa kwa wananchi wa Zanzibar hususan katika Jimbo la Wawi hasa katika Shehia ya Wawi, Gombani, Mgogoni na Kibokoni,

Je, ni lini changamoto hiyo itasahaulika katika Shehia hizo.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

179. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Hivi karibuni kutokana na maendeleo ya tehama baadhi ya vijana hususan waliopo jimboni kwangu Mwanakwerekwe wamejikita katika utaalumu wa kutengeneza mifumo mbali mbali ambayo inafaida na manufaa makubwa.

Je, Wizara ina mpango gani wa kuwatumia vijana hawa na kuwapa msukumo ili kulisaidia taifa kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia

III. HOJA ZA SERIKALI:**Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2022/2023.

Zanzibar,
20 Mei, 2022.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA